# MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA (DUWASA)






## TAARIFA YA DUWASA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA

Imeandaliwa na: -
Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
DUWASA
S.L.P 431
Email: duwasatz@yahoo.com
Simu: +255 26 2324245
Fax: +255 26 2320060
**DODOMA** **Novemba, 2015**

# TAARIFA YA DUWASA YA UTOAJI WA HUDUMA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MJINI DODOMA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 DODOMA

Mji wa Dodoma ambao ni Makao Makuu ya Tanzania upo kilometa zipatazo 450 Magharibi mwa mji mkuu wa kibiashara wa Dar es Salaam. Mkoa huu upo katika mwinuko wa meta kati ya 1030 hadi 1320 kutoka usawa wa bahari. Aidha, unapatikana katika latitudo ya $6^{o}00'$ Kusini na longitude $35^{0}45'$ Mashariki.

### 1.2 DUWASA

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ilianzishwa mwezi Julai, 1998 kwa mujibu wa kifungu na 3(1) cha sheria No.8 ya mwaka 1997 kama ilivyofanyiwa mabadiliko na sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira. Mabadiliko haya ya mwaka 2009 yaliziongezea Mamlaka jukumu la usafi wa mazingira. Hivyo kuanzia mwezi Machi 2012, Mamlaka inaitwa 'Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira' ikiwa na jukumu la msingi la kutoa huduma endelevu ya usambazaji Majisafi na usafi wa mazingira kwa wakazi wa Mjini Dodoma.

### 1.3 MUUNDO WA DUWASA

DUWASA inafanya kazi chini ya Bodi yenye Wajumbe 12 ambao huchaguliwa na Waziri mwenye dhamana ya maji. Wajumbe hao huwakilisha makundi mbalimbali kama ifuatavyo: -

- Mwenyekiti wa Bodi
- Mjumbe anayewakilisha wafanyabiashara
- Mkurugenzi wa Manispaa anayeingia kwa wadhifa wake.
- Mjumbe mwakilishi wa Serikali ya Mkoa
- Mjumbe anayewakilisha watumiaji wa maji majumbani
- Mjumbe anayewakilisha madiwani
- Mjumbe anayewakilisha wanawake
- Mjumbe anayewakilisha Wizara ya Maji
- Mjumbe anayewakilisha watumiaji wakubwa wa maji.
- Mjumbe anayewakilisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA)
- Mjumbe anayewakilisha Taasisi za Fedha (CRDB)
- Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ambaye pia ni Katibu wa Bodi.

Shughuli za kila siku za Mamlaka zinasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji anayesaidiwa kwa karibu na menejimenti. Muundo wa Mamlaka unajumuisha Idara kuu tatu za Ufundi, Biashara na Fedha na Utawala pamoja na vitengo maalumu vinavyo ripoti kwa Mkurugenzi Mtendaji moja kwa moja. Vitengo hivyo ni vya Manunuzi, Sheria, Uhusiano na Ukaguzi wa Ndani. ***Kiambatisho Na. 1*** kinaonesha muundo (*Organisation chart*) ya Mamlaka. Kwa ujumla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) ina watumishi wapatao 216 katika kada mbalimbali.

### 1.4 Dira ya DUWASA

Kuwa Mamlaka yenye ufanisi wa hali ya juu katika utoaji wa huduma ya majisafi na salama na usafi wa mazingira katika hali endelevu.

### 1.5 Dhima ya DUWASA

Utoaji wa huduma ya majisafi, salama na ya uhakika na usafi wa mazingira kwa wateja wa Mamlaka waliopo mjini Dodoma kwa ufanisi wa hali ya juu, kuwa na watumishi wenye shauku, bidii ya kazi na wanaojituma, kutumia teknolojia sahihi inayokubaliana na mazingira na kuendelea kujibidiisha zaidi ili kuongeza ufanisi na tija.

## 2.0 HISTORIA FUPI YA UPATIKANAJI WA MAJI MJINI DODOMA.

Kabla ya mwaka 1987, huduma ya majisafi mjini Dodoma ilikuwa chini ya Mhandisi wa Maji wa Mkoa (*Regional Water Engineer*) ikiwa na jukumu la kusambaza huduma ya majisafi kwa wakazi wa Mjini Dodoma. Baadaye Mwaka 1987 jukumu la usambazaji wa huduma ya majisafi lilikuwa chini ya Idara ya Maji iliyokuwa chini ya ofisi ya Mkurugenzi wa Maendeleo wa Mkoa ambapo gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uwekezaji ziligharamiwa na Serikali Kuu na huduma ya maji ilikuwa ikotolewa bila ya kuwa na msisitizo wa kuilipia kutoka kwa walionufaika. Badae mwaka 1998 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mjini Dodoma (DUWASA) ilianzishwa kusimamia jukumu la utoaji wa huduma za majisafi na uondoshaji majitaka.

Kufikia mwaka 2002, hali ya maji mjini Dodoma haikuwa ya kuridhisha kutokana na kuwepo kwa migao mikali ya huduma ya majisafi. Migao hiyo ilifanya baadhi ya maeneo kupata maji mara moja kila baada ya wiki mbili tena kwa muda mfupi sana na mengine kutopata kabisa hali iliyotishia ustawi wa mji kutokana na wawekezaji wengi kutotaka kuwekeza Dodoma.

Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwepo kwa eneo la kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo ya njia ya bomba kuu la kusafirishia maji kati ya Mzakwe na Mjini. Eneo hilo lilijulikana kama ukanda wa kijani (*green belt*). Katika eneo hili, asilimia 80 ya maji yaliyokuwa yakizalishwa yaliishia katika matumizi ya kilimo cha mizabibu, bustani, migomba n.k. Kutokana na mfumo wa kulipia flat rate uliokuwepo hapo zamani, matumizi ya maji kwa umwagiliaji katika eneo hili yalikuwa makubwa na yasiyo na kiasi.

Mara baada ya DUWASA kuanzishwa, na kwa msaada wa uongozi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ya Mkuu wa Wilaya, ilianza mikakati ya kuzuia matumizi ya majisafi kwa kilimo. Aidha ilianza mpango wa kufunga mita kwa watumiaji wote wa maji ili mteja alipie huduma ya maji kulingana na matumizi yake badala ya mfumo wa flat rate. Ufungaji mita kwa wateja wote ulikamilika mwaka 2003.

Kukamilika kwa hatua hizo kulisaidia kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa mjini Dodoma ambapo migao ya maji ilikoma, na maeneo yote yaliyokuwa hayapati maji yalianza kupata maji ya uhakika muda wote.

DUWASA ilipoanzishwa mwaka 1998, uwezo wa uzalishaji maji kutoka katika chanzo cha Mzakwe ulikuwa ni meta za Ujazo 24,000 tu. Pia DUWASA ilirithi jumla ya wateja 4,800 wa majisafi, na hapakuwa na wateja wa majitaka kwa wakati huo kwani huduma hiyo ya uondoshaji majitaka ilikuwa ikitolewa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao makuu (CDA).

## 3.0 HALI YA HUDUMA YA MAJISAFI NA UONDOSHAJI MAJITAKA MJINI DODOMA

### 3.1 Huduma ya majisafi

#### 3.1.1 Mahitaji ya maji
Utafiti na stadi za karibuni juu ya mahitaji ya maji kwa wakazi wa mji wa Dodoma ulifanywa mnamo mwaka 2002/2003 na Mhandisi mshauri SEURECA/NETWAS na kupitiwa (*reviewed*) na Mhandisi mshauri COWI Consult (2009). Kwa mujibu wa stadi hizo, mahitaji ya maji mjini kwa sasa ni wastani wa meta za ujazo 46,000 kwa siku. Kiasi hiki kinajumuisha mahitaji ya Chuo Kikuu cha Dodoma yanayofikia mita za ujazo 3,000 kwa sasa.

#### 3.1.2 Uwezo wa Uzalishaji
Chanzo pekee cha uzalishaji maji kwa matumizi ya wakazi wa mji wa Dodoma ni visima virefu vilivyochimbwa katika bonde la Makutupora. Kuna jumla ya visima vya uzalishaji maji 24 na visima vitano (5) vya kuchunguza mwenendo wa maji ardhini (*observation boreholes*). Uwezo wa visima vilivyopo kwa sasa pamoja na uwezo usafirishaji maji ni meta za ujazo zipatazo 61,500$m^3$ kwa siku.

#### 3.1.3 Usafirishaji na Usambazaji maji mjini
Kuna mabomba makuu mawili ya kusafirishia maji *(transmission mains)* kutoka kwenye chanzo eneo la Mzakwe kuja mjini yenye vipenyo vya mm 600 (inchi 24) kila moja. Mabomba hayo yana uwezo wa kusafirisha zaidi ya mita za ujazo 60,000 kwa siku kwa pamoja. Aidha, kuna vituo wiwili vikubwa vya kusukuma maji kutoka Mzakwe vinavyoweza kusukuma zaidi ya mita za ujazo 60,000 kwa siku.




*Bomba jipya la kusafirisha maji kutoka Mzakwe (Kushoto) na Kituo kipya cha kusukuma maji Mzakwe (Kulia)*

Mtandao wa kusambazia majisafi kwa sasa una jumla ya urefu wa kilomita zipatazo 393.22. Mtandao huu pia unajumuisha matenki makubwa mawili yenye ukubwa wa meta za ujazo 36,000 kila moja pamoja na matenki mengine manane (8) yanayotumika kuhifadhi na kusambaza maji yenye jumla ya meta za ujazo 20,030 hivyo kufanya jumla ya matenki yote kuwa na ujazo wa 92,030. Mtandao huu pia unajumuisha vituo sita (6) vya kusukumia maji. Jumla ya Kilomita 478 zinahitajika ili kuyafikia maeneo yote ya maji wa Dodoma. Asilimia 82 ya Wakazi wa mjini Dodoma wanapata maji ya DUWASA.



*Tanki la kuhifadhi maji Imagi (Kushoto) na kituo cha kusukuma maji Kilimani (Kulia).*

Hadi sasa, DUWASA ina jumla ya wateja 31,000 wa majisafi na jumla ya wateja 5,152 wa majitaka. Ongezeko hili la wateja limetokana na uwekezaji mbalimbali wa miradi ya majisafi na majitaka. *Chart* iliyopo hapa inaonesha mgawanyo wa wateja (*customer categories*)




## 3.2 Huduma ya majitaka

### 3.2.1 Mfumo wa kukusanya na kusafirisha majitaka

Mnamo mwaka 2002, DUWASA ilikabidhiwa dhamana ya kuendesha na kuhudumia wateja wa majitaka mjini Dodoma kutoka CDA ambapo jumla ya wateja wapatao 2,000 walikuwa wamejiunga. Mpaka sasa mtandao una urefu wa km 80.927 ambao unajumuisha mabomba makubwa ya kusafirishia majitaka (*trunk sewer & sub trunk*) yenye kipenyo cha mm 1100 na urefu wa km 24.3. na (*lateral sewers*) wenye jumla ya urefu wa km 56.627.

Mtandao huu wa kusafirishia majitaka (*Main trunk*) umesanifiwa kuhudumia watu wapatao 423,000. Hata hivyo, mtandao huu unahudumia takribani asilimia 15 tu ya wakazi kutokana na ukosefu wa mitandao midogo ya mabomba ya kukusanyia majitaka (lateral sewers). Mtandao wa mabomba ya kukusanyia majitaka (l*ateral sewers*) una jumla ya urefu wa km 56.627. Kwa mujibu wa stadi za hivi karibuni, jumla ya km 250 za mitandao ya kukusanyia majitaka zinahitajika kujengwa ili kuyafikia maeneo yote ya mji ambayo yanaweza kuunganishwa kwenye mfumo wa majitaka.

Mitandao ya kukusanyia majitaka imeenea kikamilifu (*comprehensive reticulation sewers network*) kwenye maeneo matatu ya mji. Maeneo hayo ni Mlimwa West (Area C), Mlimwa *East* (Area D) na *Central Business Area*. Maeneo mengine ya mji yaliyofikiwa na mtandao wa kukusanyia majitaka japo kwa kiasi kidogo ni kata za Makole, Viwandani, Madukani, Kizota, Chamwino, Kikuyu Kaskazini, Uhuru na Tambukareli.

### 3.2.2 Mabwawa ya kutibu Majitaka

Mfumo uliopo wa kutibu majitaka ni mabwawa (*Waste Stabilization Ponds - WSPs*) yaliyopo kilometa zipatazo sita (6) toka mjini. Mabwawa haya yapo manne (4) kila moja likiwa na ukubwa wa meta 200 X 200. Mabwawa haya yalisanifiwa kwa muda ili kuhudumia watu 68,000 tu. Kwa sasa mabwawa haya yamezidiwa kutokana na kuhudumia watu wanaozidi usanifu wake. Mpango wa kujenga mabwawa mengine ya kudumu katika eneo la Nzuguni upo katika hatua ya kutafuta fedha za ujenzi.



*Mabwawa ya kutibu majitaka yaliyopo Swaswa*

## 4.0 MIRADI MBALIMBALI YA UBORESHAJI WA HUDUMA YA MAJISAFI MJINI DODOMA

### 4.1 Mradi wa uboreshaji wa huduma za maji mjini Dodoma

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA) katika kipindi cha Januari, 2013 na Aprili, 2015 imetekeleza mradi mkubwa wa kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi kwa wakazi wa mjini Dodoma. Mradi huu umetekelezwa kwa gharama ya Dola za Marekani Milioni 49.623 ambazo zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea ambao ulitolewa kupitia Shirika lake la Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi *(Economic Development Cooperation fund* – EDCF).

### 4.1.2 Takwimu muhimu za mradi

- Mradi huu umeongeza uwezo wa uzalishaji na usafirishaji wa maji kutoka kwenye chanzo (Mzakwe) kutoka wastani wa mita za ujazo 32,000 kwa siku hadi kufikia mita za ujazo 61,500 kwa siku.
- Kazi za ujenzi wa mradi huu zimegharimu jumla ya dola za kimarekani 44.73mil/- kupitia mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea
- Mkandarasi aliyetekeleza mradi huu ni *Kolon-Hanil Joint venture* kutoka Korea na Mhandisi Mshauri ni *Saman Corporation* kutoka Korea pia.
- Mradi huu ulianza tarehe 15 Januari, 2013 na ulipangwa kukamilika tarehe 14 Januari, 2014. Hata hivyo kutokana na sababu mbalimbali zilizokuwa nje ya uwezo wa Mamlaka na Mkandarasi, mradi huu uliongezewa muda na hivyo ukakamilika mwezi Aprili, 2015.

### 4.1.3 Kazi za mradi zilizotekelezwa

- Ukarabati wa visima 17 na uchimbaji wa visima vipya viwili katika eneo la Mzakwe ili kuongeza uwezo wa uzalishaji maji hadi kufikia meta za ujazo 61,500 kwa siku.
- Ujenzi wa bomba jipya la kusafirisha maji lenye kipenyo cha kati ya 400mm na 600 mm kutoka Mzakwe hadi mjini (47.983km).
- Kuweka mfumo wa uendeshaji wa pampu za visimani na *booster stations* kutokea eneo moja *(Centralisation of boreholes and booster stations)*
- Ujenzi wa matanki mawili ya kupokelea maji katika kituo cha Mailimbili yenye yenye $790m^3$ kila moja.
- Ujenzi wa matenki mawili ya kuhifadhi maji eneo la Imagi ($7,000m^3$) na Itega ($5,500m^3$).
- Ujenzi wa maabara ya kisasa ya kupima ubora wa majisafi na majitaka pamoja na ununuzi wa mitambo/vifaa vya kisasa vya kutibu maji *(Chlorine dosing equipment)*.
- Ujenzi wa *booster stations* mpya eneo la Mzakwe na Kilimani pamoja na uboreshaji wa kituo cha kusukuma maji cha Mailimbili.
- Ulazaji wa mabomba mapya ya kusambazia maji yenye vipenyo vya kati ya 100mm na 500mm, umbali wa kilomita 32.882 kwenye maeneo ya Nzuguni, Kikuyu na Chidachi.

### 4.1.4 Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na: -

(i) Kuchelewa kuanza rasmi kwa mradi kutokana na ugeni wa Mkandarasi na Mtalaamu mshauri ambao walikuwa hawajawahi kufanya kazi katika nchi yoyote ya Afrika.

(ii) Kuchelewa kuwasili kwa vifaa mbalimbali vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi kama vile pampu, *panel* n.k

(iii) Kuchelewa kuwasili kwa mabomba ya chuma (*steel pipes*) kutoka Kampuni ya Tanzania *steel pipes* (TSP)

## 4.2 Ujenzi wa mfumo wa Majisafi na Majitaka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

Ili kuendelea kuboresha huduma za majisafi na Uondoshaji wa Majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Serikali kupitia Wizara ya Maji pamoja na wafadhili mbalimbali inatekeleza Mradi mkubwa wa kuweka miundombinu ya maji pamoja na uondoshaji majitaka inayoendana na mahitaji halisi ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2008 kwa Mhandisi Mshauri (COWI Tanzania) kufanya usanifu wa kina na kuandaa vitabu vya zabuni. Baada ya fedha za ujenzi kupatikana, Mkandarasi Sinohydro *Corporation ltd* alianza kazi mwezi Machi, 2013.

### 4.2.1 Takwimu muhimu za mradi

- Mradi una lengo la kuhakikisha huduma ya majisafi na uondoshaji majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma inakuwa ya uhakika na endelevu, na kuweza kuhudumia watu wapatao 100,000 ifikapo mwaka 2025.
- Mradi utagharimu jumla ya Shilingi bilioni 27.679 kupitia WSDP.
- Mkandarasi ni M/S SINOHYDRO kutoka China na Mhandisi mshauri ni kampuni ya COWI Tanzania ambaye pia ndiye alisanifu mradi huu.
- Ujenzi ulianza rasmi tarehe 25 Machi 2013 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 26 Novemba, 2014. Hata hivyo mkandarasi ameongezewa muda wa miezi 12 hadi mwishoni mwa mwezi Novemba 2015 kutokana na kuchelewa kwa malipo yake kutoka wizarani.

### 4.2.2 Kazi za mradi zinazotekelezwa

Kazi zinazofanyika ni kama ifuatavyo:-

**A: Kazi zilizomo kwenye Mkataba**

| **Na** | **Kazi zilizopangwa kufanyika** | **Utekelezaji** | **Kiwango cha ukamilifu (%)** |
|---|---|---|---|
| 1 | Upanuzi wa Kituo cha kusukuma maji cha Makulu pamoja na kusimika pampu tatu mpya | Kazi ya upanuzi wa jengo imekamilika. Ununuzi wa *Pumps* tatu (3) na ufungaji umekamilika lakini bado hajafanya *testing*. | 85 |
| 2 | Ujenzi wa bomba la kusafirisha maji lenye kipenyo cha 315mm na 355mm HDPE kwa urefu wa 15.695km | Ujenzi wa umekamilika | 100 |
| 3,4,5 | Ujenzi wa matanki matatu ya kuhifadhi maji kwenye vilima vya Chimwaga (4,500$m^3$), Informatics (3,000$m^3$) na Luangu (4,500$m^3$) | **Tanki la Chimwaga:** Kazi za ujenzi zimekamilika na tanki hilo tayari linatumika. | 100 |
| | | **Tanki la *Informatics***: Kazi za ujenzi zimekamilika na tanki hilo tayari linatumika. | 100 |
| | | **Tanki la Luangu**: Kazi za ujenzi zimekamilika na tanki hilo tayari linatumika. | 100 |
| 6 | Ujenzi wa mabomba ya kusambazia maji yenye vipenyo vya 75mm mpaka 250mm HDPE kwa urefu wa 9.642km | Jumla ya kilomita 9.81 za mabomba tayari zimelazwa. | 100 |
| 7 | Ujenzi wa mabwawa ya Kutibu Majitaka. | Ujenzi wa mabwawa ya *anaerobic* (2units), *Facultative* (2units) na *Maturations* (4units) umekamilika. | 100 |
| 8 | Mtaro wa maji ya mvua (*Open Channel drain*), 1679.8m length. | Ujenzi wa mtaro umekamilika | 100 |
| 9 | Ujenzi wa mfumo wa mabomba ya majitaka kwa kulaza mabomba ya kusafirisha majitaka yenye urefu wa kilomita 17.09 pamoja na mabomba ya kukusanyia majitaka yenye urefu wa kilomita 6.5. Pia mabomba madogo yenye urefu wa kilomita 8. | Ujenzi wa Bomba kuu la kusafirisha majitaka umekamilika. Maunganisho kwenye colleges mbalimbali yanaendelea | 95 |
| | **Kwa wastani, mradi umekamilika kwa asilimia** | | **97.7** |

**B: Kazi za nyongeza**

| Na. | Kazi zilizoongezwa | Utekelezaji wake | Kiwango cha ukamilifu (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa tanki la kupokelea maji (Sump) eneo la Makulu lenye uwezo wa 2,500$m^3$ | Ujenzi wa tanki umekamilika na tayari limeanza kutumika | 100 |
| 2 | Ujenzi wa mfumo mpya wa uondoshaji majitaka katika *college* ya *Humanities,* 3.9km. | Mkandarasi anamalizia maeneo ya makorongo ambayo yalikuwa yanasubiri bomba za GRP.<br><br>Bomba hizo zimewasili mwezi Juni, 2015 baada ya Mkandarasi kulipwa IPC Na.7 | 92 |
| 3 | Upanuzi wa kibanda cha kufungia *transforma* pamoja na ujenzi wa *fence* ya tofali kuzunguka kituo cha Makulu | Upanuzi wa Kibanda umekamilika. Ujenzi wa *fence* utaanza hivi karibuni. | 40 |
| 4 | Ununuzi na Usimikaji wa *Transformer*, *swith gear* na *Isolator* katika Kituo cha Makulu | Vifaa vyote vimenunuliwa na ukaguzi umefanyika. Kazi za ufungaji zimekamilika. | 95 |
| 5 | Ujenzi wa mtambo maalumu wa kutibu majitaka katika *college* ya Afya (UDOM). | Kazi hii ipo kwenye hatua ya usanifu. | 10 |
| 6 | Ujenzi wa mfumo wa uondoshaji majitaka kutoka kwenye eneo lililopendekezwa kujengwa nyumba za watumishi UDOM | Kazi za upimaji (*survey*) zinaendelea | 5 |
| 7 | Ujenzi wa vibanda vinne (4) vya walinzi kwenye matanki ya maji pamoja na Mabwawa ya majitaka. | Michoro imeandaliwa na kazi zitaanza hivi karibuni. | 5 |
| | **Kwa wastani, kazi za nyongeza zimekamilika kwa asilimia** | | 49.6% |

*Note: Kazi za nyongeza hazitekelezwi kwa kasi inayotakiwa kutokana na kuchelewa kwa malipo ya Mkandarasi.*

4.2.3: Changamoto

Changamoto kubwa zinazojitokeza katika utekelezaji wa mradi huu ni: -

(i) kuchelewa kwa malipo ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri, hali inayosababisha kupunguza kasi ya utekelezaji wa mradi.

(ii) Kuwepo kwa mabadiliko makubwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma tangu mradi uliposanifiwa mwaka 2008, ikilinganishwa na kuanza kwa utekelezaji wake mwaka 2013. Wakati wa Usanifu, Mhandisi Mshauri hakujua mahali halisi palipopangwa kujengwa baadhi ya majengo, na hivyo kutoyajumuisha kwenye usanifu. Hali hii imelazimu kuwepo kwa kazi nyingi za nyongeza ili kukidhi mahitaji ambayo hayakubainishwa kipindi cha usanifu.

**4.3 Mradi wa Chanzo cha Maji cha Farkwa –Wilaya ya Chemba**

Mradi wa ujenzi wa Bwawa la maji katika tarafa ya Farkwa iliyopo wilaya mpya ya Chemba una lengo la kupata chanzo cha nyongeza cha maji kwa wakazi wa mjini Dodoma.

Kazi ya tathmini ya athari za mazingira na Kijamii (ESIA) zinazofanywa na Mtaalam mshauri *Tres Consult ltd* kutoka Tanzania zimekamilika. Wizara ya Maji iliitisha kikao cha wadau cha kupitia taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii (ESIA) tarehe 30/07/2015 katika ukumbi wa St. Gasper mjini Dodoma.

Aidha, kazi za Usanifu wa Bwawa hilo pia zimekamilika. Mhandisi Mshauri M/S TRACTEBEL Engineering kutoka Ufaransa amewasilisha *Draft Final report* ambayo ilipitiwa na jopo la wataalam (*Panel of experts*) jijini Dar Es Salaam tarehe 3-4/09/2015.

Pia, mnamo tarehe 07/10/2015, Wataalam wa Wizara ya Maji waliambatana na Wataalam wa TANROAD na TANESCO kwenda Farkwa ili kuoneshana sehemu ya barabara na miundombinu ya TANESCO itakayoathirika na ujenzi wa Bwawa na mahali pa kuihamishia.

Kwa mujibu wa Wizara ya maji, kazi za ujenzi wa mradi zitaanza mwishoni mwa mwaka wa fedha 2015/2016.

## 5.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI DUWASA

Katika utekelezaji wa kazi za kila siku, DUWASA ina changamoto zifuatazo: -

- Taasisi za Serikali kutolipia ankara zake za maji kwa wakati. Hadi mwezi Oktoba, 2015, DUWASA inadai jumla ya Tshs. 800mil/ kutoka Taasisi za Serikali pekee.

- Ufinyu wa mtandao wa kusambazia maji. Hadi mwezi Oktoba, 2015, mtandao wa majisafi una urefu wa kilometa 393.22 tu ukilinganisha na mahitaji ya takribani kilometa 478. Pia urefu wa mtandao wa majitaka ni kilometa 81 tu ikilinganishwa na takribani kilometa 250 zinazohitajika.

- Upotevu wa maji umeongezeka kutoka wastani wa 28% mwezi Mei, 2015 na kufikia wastani wa 30% mara baada ya kuanza kutumika kwa mradi mpya mwezi Juni, 2015.

  Juhudi mbalimbali zinafanyika ikiwa ni pamoja na kuimarisha kikosi cha kuzuia uvujaji wa maji pamoja na kubadilisha mita za maji za siku nyingi ili kupunguza upotevu wa maji.

- Gharama kubwa za umeme, ambazo sasa zinafikia 300mil/- kwa mwezi.

- Kukatika kwa umeme mara kwa mara katika mitambo ya uzalishaji maji na hivyo kusababisha uzalishaji maji kusimama.

## 6.0 HITIMISHO

- DUWASA inatoa shukurani nyingi kwa wadau wake wote kwa ushirikiano ambao wameendelea kuipatia. Aidha, tunaomba ushirikiano huo uendelee ili huduma ya majisafi na Majitaka kwa wakazi wa mjini Dodoma iwe endelevu.

“MAJI KWA MAISHA SALAMA”

DUWASA ORGANIZATION CHART

